# MIFUMO YA TEHAMA YAIMARISHA UTENDAJI KAZI KATIKA MANISPAA YA KIN0NDONI.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilikuwa ya kwanza kujidhatiti na kutekeleza kwa vitendo agizo la Serikali kuu la kutumia mifumo ya Kielectroni katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi serikalini kwa kuhakisha huduma zinazotolewa kwa wanachi zinakuwa bora na kutolewa kwa haraka na kwa wakati jambo lililoifanya kuwa Manispaa ya mfano Tanzania na Afrika kwa kupata nishani ya Halmashauri bora.

Katika kuhakikisha inajiletea kikamilifu maendeleo yake, Manispaa ya Kinondoni iliamua kuanzisha utaratibu maalumu wa kuimarisha mifumo ya TEHAMA itakayowezesha kukusanya mapato kwa kutumia tekinolojia hii, hatua iliyowezesha kuleta mafanikio ya haraka kutokana na mapato yanayokusanywa kila mwaka kuongezeka na huduma zinazotolewa kwa wananchi kuwa za ufanisi, ubora, za haraka na kwa wakati na kuwawezesha wananchi kufurahia huduma hizo katika kila sekta ya Manispaa iliyoimarishiwa mifumo.

Kimsingi mifumo hii imerahisisha utendaji kazi katika sekta zote katika Manispaa ya Kinondoni na kuweka uwazi katika utekelezaji wa kazi na shughuli mbalimbali jambo lililowawezesha wananchi kushiriki katika maamuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayoihusu Manispaa yao hususani ukusanyaji wa mapato na matumizi yake kwani taarifa zote muhimu zinapatikana kwa haraka na kwa wakati.

Ni wazi kabisa kuwa kabla ya uwepo wa mifumo hii ya TEHAMA shughuli nyingi za utoji huduma katika sekta mbalimbali za Manispaa ya Kinondoni zilikumbana na changamoto mbalimbali zilizokuwa kikwazo katika harakati za kuwaletea wananchi maendeleo. Huduma hazikuwa zinapatikana kwa wakati na kwa haraka na hivyo kuathiri ubora na ufanisi wake jambo lililosababisha malalamiko kutoka kwa wananchi wake.

Kwa mfano katika suala zima la ukusanyaji wa mapato lilikuwa linamlazimisha mlipaji kutembea mwendo mrefu jambo liliosababisha wananchi wengi kutolipa mapato ya Manispaa kutokana na changamoto za usafiri(foleni) na usumbufu wa huduma inayotolewa na wataalamu kwa mikono(manual) iliyosababisha mlipakodi mmoja kutumia muda mrefu kupata huduma na kusababisha misongamano ya watu katika maeneo ya kutolea huduma hiyo.

Changamoto nyingine ni pamoja na udhaifu katika utunzaji wa taarifa na takwimu mbalimbali jambo lilopelekea kuwa na taarifa na takwimu zisizosahihi na hivyo kutokuwa na maamuzi sahihi katika sekta mbalimbali kutokana na kukosa taarifa sahihi. Hii ni pamoja na kushuka kwa kiwango cha mapato ya Manispaa mwaka hadi mwaka na kudhoofisha kiwango cha huduma za maendeleo zinazotolewa na Manispaa mambo ambayo yamedhibitiwa kutokana na kuwekeza katika mifumo.

Kwa sasa wakazi wa Kinondoni wanapata taarifa kila wakati kutoka Manispaa ya Kinondoni kwa kutumia mifumo ya TEHAMA kupitia tovuti ya Manispaa www.kinondonimc.go.tz, na kupitia mitandao ya kijamii kama vile facebook, twiter, instagram, you Tube, blogs na online Tv ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekuwa ikitoa taarifa mbalimbali za kisekta. Pia Manispaa ya Kinondoni imejiunga katika mfumo wa barua pepe ambapo watumishi wote hupashana habari kupitia email zao.

Kwa namna ya Pekee Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ina kila sababu ya kutambua na kuthamini mchango wa wakala ya Serikali Mtandao (ega) kwani wamekuwa nyuma ya mafanikio yetu kwa kuhosti tovuti ya Manispaa kwa gharama nafuu na kuondokana kabisa na tatizo la tovuti kutopatikana .Pia ega wameweza kutupatia huduma ya internet kwa kushirikiana na TTCL kwa gharama nafuu katika mradi wa RCIP ambapo Manispaa ya Kinondoni ilikuwa ya kwanza kuwa na huduma ya Free wifi katika kituo cha Simu 2000 ambacho kwa sasa kiko chini ya Manispaa ya Ubungo baada ya kugawanyika, kitaalamu kwa Manispaa ya

Kinondoni kuhusa matumizi sahihi ya TEHAMA, jinsi ya kuwezesha usalama wa kimtandao (cyber security) sambamba na kutoa mafunzo mbalimbali katika Manispaa ya Kinondoni. Hivyo kwetu ega imekuwa ni kiungo muhimu kati ya Manispaa na Serikali kuu katika masuala yote ya TEHAMA.

Kwa kuzingatia ukweli kuwa mifumo ya TEHAMA imewasaidia sana Wananchi wa Manispaa ya Kinondoni kwani ongezeko la mapato la mwaka hadi mwaka yanayokusanywa na Manispaa ya Kinondoni huelekezwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo yenye manufaa kwa wananchi kama ujenzi wa madarasa, barabara madaraja, mifereji ya maji ya mvua huduma za kiafya na mambo kadha wa kadha ambazo hutolewa kwa ubora wa kiwango cha juu.

Hii pia inatokana na ukweli kuwa uwepo wa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za mapato ya Manispaa (LGRCIS) Umewezesha Manispaa kuwa na takwimu sahihi za walipakodi, ongezeko la mapato yanayokusanywa, na uwepo wa mazingira mazuri ya wananchi kuja kulipa kodi bila shuruti (tax comp-lience).

Mwisho Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kutambua umuhimu wa TEHAMA katika mafanikio yake imeamua kujidhatiti katika kuwekeza kwa kiwango kikubwa kwenye uimarishaji wa mifumo kwa kuanzisha matawi katika maeneo mbalimbali katika kata kama Mwenge, Mikocheni, Tegeta, Bunju, Mbweni na Mabwepande sambamba na kuondoa changamoto ya upatikanaji wa internet kwa kuweka buckup system ya umeme na cyberben opphen ambayo inagawanya internet katika njia mbalimbali na kuondoa matumizi yasiyokubalika  nyakati za kazi.